# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA

## WIZARA YA KILIMO

## BODI YA KOROSHO TANZANIA

**MWONGOZO NA. 2 WA USIMAMIZI NA UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI WA MWAKA 2021/2022 TOLEO LA 4**

**MWONGOZO HUU UMETOLEWA CHINI YA SHERIA YA TASNIA YA KOROSHO NA. 18 YA MWAKA 2009 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2010**

Umetolewa na:-
Bodi ya Korosho Tanzania
S. L. P. 533
MTWARA

SEPTEMBA, 2021

# YALIYOMO


SEHEMU YA KWANZA........................................................................................................ 1

1.0 UTANGULIZI.................................................................................................................... 1

SEHEMU YA PILI .................................................................................................................. 2

2.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI NGAZI YA MKULIMA ........................................... 2

SEHEMU YA TATU ................................................................................................................ 3

3.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA NGAZI YA CHAMA CHA USHIRIKA CHA MSINGI.......................................................................................................................... 3

SEHEMU YA NNE .................................................................................................................. 4

4.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA GHALA LA MNADA ................................... 4

SEHEMU YA TANO................................................................................................................ 8

5.0 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU KATIKA KUSIMAMIA UBORA WA KOROSHO GHAFI 8

SEHEMU YA SITA................................................................................................................. 11

6.0 UTATUZI WA MIGOGORO ................................................................................................. 11

# 1 TAFSIRI YA MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| ***AMCOS*** | ni Chama cha *Ushirika* cha Msingi. |
| ***Chama Kikuu*** | ni Chama Kikuu cha Ushirika. |
| ***Cutting test*** | ni kupima ubora wa Korosho-karanga (kernel) baada ya Korosho ghafi kukatwa. |
| ***First in First Out*(FIFO)** | ni mfumo wa utoaji wa korosho kwa kuzingatia Korosho zitakazoanza kuingizwa ghalani ziwe za kwanza kutolewa ghalani. |
| ***Ghala la Chama cha Ushirika cha Msingi*** | ni ghala la kukusanyia Korosho za wakulima kwa ajili ya kuzipeleka katika ghala la mnada. |
| ***Ghala la mnada*** | ni ghala lililokidhi sifa na vigezo kwa ajili ya kupokea Korosho za wakulima zinazosubiri kuuzwa kwa mnada. |
| ***Kanuni*** | ni kanuni za Tasnia ya Korosho ya mwaka 2010. |
| ***LBS*** | ni Kipimo cha uzito katika ratili. |
| ***Loti*** | ni fungu la Korosho zilizopo katika ghala la mnada zinazosubiri kuuzwa kwenye mnada. |
| ***Mchanganuo wa Mauzo (Sales catalogue)*** | ni kijarida cha taarifa ya Korosho ghafi kinachoonesha namba ya stakabadhi, tarehe ya stakabadhi, mmiliki, kiasi, idadi ya magunia, ubora, loti, namba ya mnada na ghala la mnada. |
| ***Mfumo wa stakabadhi za Ghala*** | ni mfumo wa soko ambapo Korosho huwekwa katika ghala na kutolewa stakabadhi ikionesha kiasi, ubora na daraja la Korosho kwa lengo la kusubiri kuuzwa. |
| ***Mnunuzi*** | ni mfanyabiashara aliye na leseni ya ununuzi wa Korosho kutoka Bodi ya Korosho Tanzania katika msimu husika |
| ***Msafirishaji*** | ni msafirishaji wa Korosho kutoka ghala la AMCOS hadi ghala la mnada na kutoka ghala la mnada kwenda ghala la mnunuzi/bandarini |
| ***Mtaalam wa Ubora*** | ni mtaalam aliyefuzu mafunzo ya uhakiki ubora wa Korosho na kupata cheti kutoka Bodi ya Korosho Tanzania na kuajiriwa na mwendesha ghala kwa ajili ya kuhakiki ubora waKorosho zinazoingia ghala la mnada. |
| ***Mwendesha ghala*** | ni mtu/kampuni aliyepata/iliyopewa leseni kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa ajili ya upokeaji, |

utunzaji na utoaji wa Korosho ghafi kutoka katika ghala la mnada.

***Nut count"*** ni idadi ya Korosho ghafi katika kilo moja ya Korosho.

***PDN* (Produce Dispatch Note)** ni hati ya kusafirisha Korosho ghafi ndani ya nchi.

***Shelling out turn*** ni kiasi cha Korosho-karanga zinazopatikana baada ya kubangua gunia la korosho ghafi lenye uzito wa kilo themanini na huwasilishwa (presented) kwa ratili .

***Sheria"*** ni sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009.

***TBS"* (Tanzania Bureau of Standards)** ni Shirika la Viwango Tanzania.

***w/w"*** Uzito wa unyevu uliomo katika mzigo wa korosho.

***WMA"*** ni Wakala wa Vipimo Tanzania.

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

Mwongozo huu umetolewa chini ya sheria Na.18 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010 kifungu cha 59.

Mwongozo huu unatakiwa kusomwa sambamba na sheria ya Tasnia ya korosho Na. 18 ya mwaka 2009 (sura ya 203 ya Sheria za Tanzania) pamoja na kanuni zake za mwaka 2010 (Tangazo la serikali Na.420 la mwaka 2010). Atakayekiuka matakwa ya mwongozo huu atakuwa anatenda kosa hivyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

Mwongozo unatoa maelekezo juu ya utaratibu wa usimamizi na udhibiti ubora wa korosho ghafi wa mwaka 2021/2022.

Kwa kushirikiana na wadau mahsusi wa Tasnia ya Korosho, Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa Mwongozo huu kuwezesha wadau mbalimbali kujua taratibu zitakazotumika katika kusimamia ubora wa Korosho ghafi kwa msimu wa 2021/2022. Aidha, majukumu ya kila mdau anayopaswa kutekeleza kuanzia ngazi ya mkulima hadi bandarini yameainishwa ndani ya Mwongozo huu.

### 1.2 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ngazi ya Chama cha Ushirika cha Msingi

Mtaalamu wa ubora katika ngazi ya Chama cha Ushirika cha Msingi anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

1.2.1 Awe amepata mafunzo ya udarajishaji wa msingi wa Korosho ghafi.
1.2.2 Awe mkulima mzoefu.
1.2.3 Awe mjumbe wa Bodi au mtendaji wa Chama cha Msingi cha Ushirika husika.
1.2.4 Awe amehudhuria mafunzo ya ubora au semina kabla ya msimu husika.

### 1.3 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ghala la mnada

Mtaalamu wa ubora atakayeajiriwa na mwendesha ghala anapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

1.3.1 Awe na elimu angalau ya astashahada ya kilimo au taaluma nyingine yoyote inayoshabihiana na kilimo.
1.3.2 Awe amepata mafunzo ya uhakiki/udhibiti ubora wa korosho ghafi na cheti kutoka Bodi ya Korosho.
1.3.3 Awe ni muadilifu katika utendaji wa kazi za uhakiki ubora.
1.3.4 Iwapo atakuwa na uzoefu (sifa ya ziada) wa kufanya kazi katika misimu

iliyotangulia awe na historia nzuri ya utendaji kazi na uadilifu kutoka kwa mwajiri wa awali na kuhudhuria semina za maandalizi ya kuanza msimu husika.

1.3.5 Awe amesajiliwa na kupata kibali cha kufanya kazi ya uhakiki ubora kutoka Bodi ya Korosho Tanzania baada ya kupata mkataba wa kazi kutoka kwa mwendesha ghala.

1.3.6 Mtu yeyote atakayegundulika kufanya kazi za uhakiki ubora ghala la mnada bila kuwa na sifa tajwa hapo juu na hajasajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania atawajibika kwa mujibu wa kifungu cha 20(4) cha Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI NGAZI YA MKULIMA

### 2.1 Uvunaji Korosho Ghafi

2.1.1 Korosho inapaswa kukomaa ikiwa juu ya mti wa mkorosho na kabla ya Korosho kudondoka chini mkulima anapaswa kuhakikisha eneo la mzunguko wa matawi ya mkorosho ni safi.

2.1.2 Mkulima anapaswa kuokota Korosho zilizokomaa na kudondoka zenyewe na si kuzichuma au kuzitikisa mti ili zidondoke.

2.1.3 Baada ya kuokota Korosho, mkulima anapaswa kutenganisha bibo na Korosho kwa kuizungusha Korosho mpaka inaachana na bibo. Endapo mkulima ana aina ya mikorosho ambayo vipande vya mabibo vinang'ang'ania na kubakia kwenye Korosho baada yakutenganishwa na mabibo, atapaswa kuviondoa vipande hivyo kwa kutumia kisu. Kazi hiyo ifanyike kwa uangalifu kuepuka kuitoboa Korosho kwenye sehemu ambayo bibo linajishika.

2.1.4 Mkulima anapaswa kuokota Korosho angalau mara 3 kwa wiki zinapoanza kudondoka na kila siku wakati korosho zinapokomaa kwa wingi na kama kuna mvua ziokotwe kila siku kuepuka kupotea kwa ubora.

### 2.2 Uanikaji wa Korosho Ghafi

2.2.1 Korosho zianikwe juani kwa muda wa siku 3-4 mfululizo zikigeuzwageuzwa. Ni vyema Korosho zianikwe katika sakafu nzuri, jamvi, vitanga, mikeka au maturubai.

2.2.2 Korosho zianikwe hadi zikauke vizuri. Korosho zilizokauka vizuri zina sauti kali inayosikika "rattling sound" kama zitadondoshwa kwenye sakafu ya saruji au kuchezeshwa kwenye viganja.

2.2.3 Ili kujiridhisha na kiwango cha unyevu kifaa cha kupima unyevu kitumike na unyevu usizidi asilimia 10.

### 2.3 Uchambuaji (Sorting)

2.3.1 Mkulima anatakiwa kutenganisha korosho na vitu visivyo korosho kama vile mabaki ya mabibo makavu (kochoko), majani ya miti, nafaka na mazao mengine, kokoto, mawe mchanga n.k. Kuondoa korosho zilizooza, korosho zisizokomaa, korosho ndogo sana na korosho zilizotoboka au kuanza kuota.

2.3.2 Mkulima akipeleka Korosho chafu ambazo hazijachaguliwa au hazijakauka vizuri kwenye ghala la Chama cha Msingi atawajibika kwa gharama zozote zitakazohitajika kuboresha au kudarajisha Korosho hizo.

2.3.3 Mkulima atakayegundulika kuruhusu, kusababisha au kuweka mchanga au kitu kisicho Korosho ilikuongeza uzito na kuchanganya korosho zisizo na ubora za misimu iliyopita kupeleka ghala la chama cha msingi atawajibika kwa mujibu wa

sheria Na.18 ya mwaka 2009 kifungu cha 23(a) na Muongozo huu.

### 2.4 Kuhifadhi Korosho Ghafi

2.4.1 Korosho zilizokauka na kuchambuliwa zihifadhiwe vizuri kabla ya kupelekwa ghalani.

2.4.2 Korosho inapaswa kuhifadhiwa sehemu kavu, isiyovuja na yenye hewa ya kutosha. Korosho zisipokaushwa vizuri zinaweza kuharibika, kuota au kuoza kabisa ndani ya muda mfupi wa uhifadhi.

## SEHEMU YA TATU

**3.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA NGAZI YA CHAMA CHA USHIRIKA CHA MSINGI**

3.1 Karani wa AMCOS au mjumbe wa Bodi anayehusika na ubora anapaswa kukagua korosho za mkulima na kuhakikisha kwamba zimekauka, zimechambuliwa na hazijachanganywa na vitu visivyo korosho (mchanga, mawe, kochoko n.k).

3.2 Mtaalamu wa ubora wa AMCOS anapaswa kukagua kama korosho zimekauka vizuri na zimechambuliwa vizuri kwa mkulima mmoja mmoja kabla ya kupokelewa katika ghala la Chama cha Msingi. Kwa AMCOS ambazo zitapata vifaa vya ubora vya awali watatumia kipima unyevu wa korosho na mizani ndogo kukagua idadi ya korosho kwa kilo (kama korosho zimechaguliwa vizuri) kabla ya kupokea korosho ghalani .

3.3 Baada ya ukaguzi korosho zipimwe uzito na kuwekwa katika gunia la mkonge/kitani lenye alama za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho Na.1 na kuhifadhiwa ghala la Chama cha Msingi.

3.4 Gunia za korosho zinapaswa kuhifadhiwa kwenye ghala lisilovuja, linaloruhusu mzunguko wa hewa na kupangwa juu ya magogo, mbao au chaga "pallet" ili kutunza ubora.

3.5 Gunia la kuhifadhi korosho linapaswa kuwa la mkonge/ kitani lenye ubora uliopitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lenye uwezo wa kuhifadhi kilo 80 za Korosho ghafi.

3.6 Wakati wa upakiaji wa Korosho watendaji wa Chama cha Msingi, msindikizaji na msafirishaji wanapaswa kujiridhisha kama korosho zimefanyiwa ukaguzi wa awali na uzito wa Korosho. Iwapo kutatokea tofauti ya uzito kati ya uliopimwa ghala la chama cha msingi na ghala la mnada na ikathibitika upungufu huo, msindikizaji na kampuni ya usafirishaji atawajibika kulipa gharama ya kiasi kilichopungua.

3.7 Chama cha Ushirika cha Msingi kitakachopeleka korosho ambazo hazijakidhi viwango kwenye ghala la mnada kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 4.4.4 kwenye mwongozo huu, korosho hizo hazitaruhusiwa kutoka nje ya ghala hadi itakapothibitika ufinyu wa nafasi katika ghala husika. Chama cha Msingi kitawajibika kwa gharama zozote zitakazohitajika kuboresha korosho hizo.

3.8 Viongozi/Watendaji wa Chama cha Ushirika cha Msingi watakaobainika kuchanganya korosho na vitu visivyo korosho au korosho zisizokidhi viwango vya ubora ili kuongeza uzito na kupeleka ghala la mnada watawajibika kwa mujibu wa Sheria za nchi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA GHALA LA MNADA

### 4.1 Taratibu za Kuingiza Korosho Ghala la mnada

4.1.1 Korosho zitakazopelekwa kwenye ghala la mnada zitahakikiwa na kuthibitishwa ubora kulingana na viwango vilivyoainishwa katika mwongozo huu kabla ya kupokelewa ghalani na kuandaliwa kwa ajili ya mnada kwa kuzingatia Mwongozo wa pamoja wa mauzo msimu wa korosho wa mwaka 2021.

4.1.2 Korosho zitapokelewa katika ghala la mnada kwa madaraja yote mawili "daraja la kwanza na daraja la pili" wakati wote wa msimu. Korosho daraja la kwanza na daraja lapili zipangwe katika loti tofauti.

4.1.3 Korosho ghafi ambazo hazijakidhi viwango vya ubora kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 4.4.4 katika mwongozo huu, viongozi wa AMCOS washauriwe kuboresha korosho hizo ghalani ili kufikia vigezo vya ubora. Kama korosho hazitakidhi zihifadhiwe katika ghala kwa makubaliano maalumu na itolewe stakabadhi ya korosho mbovu zinazobaki ghalani. Baada ya msimu kukamilika maelekezo ya korosho hizo zilizokamatwa yatatolewa ili kuepuka uchanganyaji wa korosho nzuri na zisizokidhi vigezo.

4.1.4 Taratibu zote za kuhakiki ubora wa korosho zinazopokelewa kwenye ghala la mnada utafanywa na mtaalam wa mwendesha ghala mbele ya mwakilishi wa AMCOS na kuweka kumbukumbu sahihi za matokeo ya uhakiki huo kwa mujibu wa taratibu za kupokea korosho kwenye ghala la mnada.

4.1.5 Vyama Vikuu vya Ushirika vitaruhusiwa kuajiri wataalamu wa ubora waliopata mafunzo na cheti cha uhakiki ubora kutoka Bodi ya Korosho watakaosimama kwaniaba ya AMCOS katika ghala la mnada kuhakikisha kuwa upimaji ubora wa korosho zinazopokelewa unafanyika kwa kuzingatia taratibu zote za uhakiki ubora.

### 4.2 Utaratibu wa Kuchukua Sampuli

Hatua ya msingi katika zoezi la uhakiki ubora wa Korosho ghafi ni jinsi ya upatikanaji wa sampuli. Mtaalamu wa ubora anapaswa kuzingatia hatua zifuatazo wakati wa uchukuaji wa sampuli.

4.2.1 Sampuli itolewe kwa uangalifu kwa kutumia sampuli nasibu "random sampling" kutoka katika mzigo wa Korosho ghafi.

4.2.2 Kifaa maalumu cha kuchukulia Sampuli kitatumika kuchukua sampuli kutoka pande zote nne na katikati kwa kila gari litakalopeleka mzigo ghala la mnada.

4.2.3 Sampuli inapaswa iwe ya kweli na iliyochukuliwa kutoka katika gari husika (representative sample).

4.2.4 Sampuli inayopaswa kuchukuliwa si chini ya asilimia 50% ya magunia yote yaliyo kwenye gari, kwa kutegemea ukubwa wa mzigo na idadi ya gunia zitakazohakikiwa. Sampuli inavyokuwa kubwa na usahihi wa matokeo unaongezeka.

4.2.5 Iwapo mtaalamu wa uhakiki ubora atagundua kasoro au kuwa na wasiwasi wowote kuhusu ubora wa mzigo uliobebwa kwenye gari husika anapaswa kuchukua sampuli ya mzigo wote (100%) ili kujiridhisha na usahihi wa uhakiki

ubora atakaofanya. Iwapo itagundulika kuna kitu chochote kisicho korosho kama mchanga, mawe, kokoto na vinginevyo, korosho zote zishushwe na kukaguliwa na taarifa itolewe kwa vyombo husika kwa hatua zaidi.

4.2.6 Iwapo itagundulika kuna unyevu wa kiwango cha juu kwenye magunia yaliyofungashiwa korosho, gari zima likaguliwe na magunia yatakayobainika kuwa na changamoto ya unyevu yashushwe na korosho zianikwe na kuchambuliwa ili zikidhi vigezo vya ubora kabla ya kupokelewa ghalani kwa mujibu wa mwongozo huu.

4.2.7 Gari lililofunikwa kote (box body truck) litakalopeleka mzigo ghalani ni lazima magunia yote ya Korosho yashushwe chini kisha sampuli ichukuliwe kwa ajili ya zoezi la uhakiki ubora.

4.2.8 Sampuli itakayochukuliwa ili kuhakiki ubora inatakiwa iwe na unyevu usiozidi asilimia kumi (10%) ili mzigo upokelewe ghalani.

4.2.9 Sampuli ichanganywe vizuri kisha ipimwe na wastani wa sampuli katika zoezi la uhakiki uborawa korosho ghafi "cutting test" ni kilo moja.

## 4.3 Vifaa Vinavyohitajika Katika Zoezi la Uhakiki Ubora

i. Kipima unyevu (moisture meter) kilichofanyiwa ugezi "calibration" na TBS (kipima unyevu kinachoshauriwa ni Steinlite SB 900)
ii. Mkasi wa kukatia Korosho
iii. Bisibisi au chuma ya baiskeli (scooper)
iv. Mizani ndogo ya kidijitali ithibitishwe na WMA
v. Kifaa maalum cha kuchukulia sampuli
vi. Kikokotoo (calculator), kalamu na daftari dogo
vii. Mafuta ya nazi au nyonyo au "gloves"
viii. Bakuli au sahani zenye rangi tofauti
ix. Tishu au kitambaa maalumu
x. Meza ya kukatia sampuli na chombo (ndoo au gunia) cha kubebea sampuli.

## 4.4 Taratibu za Kupima Sampuli

Mtaalamu wa Ubora anapaswa kufuata taratibu zifuatazo wakati wa kupima sampuli ya Korosho ghafi.

4.4.1 Sampuli ipimwe asilimia ya unyevu "moisture content" kwa kutumia kifaa maalumu kiitwacho kipima unyevu "moisture meter". Kiwango cha unyevu kinapaswa kisizidi asilimia kumi 10% (w/w). Iwapo Korosho hazitakidhi kiwango hiki cha unyevu, kipengele 4.1.3 cha Mwongozo huu kitumike.

4.4.2 Sampuli ipimwe kilo moja na kuhesabiwa idadi ya Korosho kwa kilo (nut count). Kipimo hiki hutegemea ukubwa na uzito wa Korosho katika kilo moja na idadi ya Korosho haipaswi kuzidi mia mbili (200). Iwapo Korosho hazitakidhi kiwango kipengele 4.1.3 cha Mwongozo huu kitumike.

4.4.3 Korosho zilizohesabiwa zikatwe kwa kutumia mkasi maalum wa kukatia Korosho ghafi kisha ziwekwe mafungu tofauti kwa Korosho zilizokatwa kama ifuatavyo:-

GN – "Good kernels" (Korosho karanga nzuri)
IMM –"Immature kernels" (Korosho karanga zisizokomaa)
SP –"Spotted kernels" (Korosho karanga zenye madoa)

PD – "Partial damaged" (Korosho zilizoanza kuoza)
Kisha njia ifuatayo itumike kutafuta "Shelling Out Turn"

$$SHOT = \left\{GN + \frac{(IMM+SP+PD)}{2}\right\} \times 0.176$$

4.4.4 Madaraja ya Korosho ghafi yanayotambulika kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 na kanuni ya 26 ya kanuni za Tasnia ya Korosho za mwaka 2010, ni daraja la kwanza na daraja la pili.

**Daraja la kwanza**
SHOT= 48lbs/80kg bag na zaidi (≥ 48 lbs/80kgbag).
Unyevu wa Korosho "Moisture content" inapaswa isizidi asilimia kumi 10% (w/w). Idadi ya Korosho kwa kilo moja "Nut count" inapaswa isizidi mia mbili (200).

**Daraja la pili**
SHOT = (44lbs/80kg bag – 47 lbs/80kg bag).
Unyevu wa Korosho "Moisture content" inapaswa isizidi asilimia kumi 10% (w/w).Idadi ya Korosho kwa kilo moja "Nut count" inapaswa isizidi mia mbili (200).

4.4.5 Korosho zenye ukungu kwa nje aidha wa rangi nyeupe, kijani, nyeusi au njano zisipokelewe kwenye ghala la korosho kuanzia ngazi ya AMCOS hadi ghala kuu. Wakulima wazingatie kutenganisha vizuri korosho na bibo na kukausha korosho vizuri kuepuka changamoto hii.

4.4.6 Mtaalamu wa ubora wa ghala la mnada atakapobainika kukiuka taratibu za uhakiki ubora zilizoainishwa kwenye mwongozo huu na kusababisha uwepo wa Korosho zisizokidhi viwango ghalani. Mtaalamu huyo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutoruhusiwa kusimamia ubora katika ghala za mnada kwa kipindi cha misimu mitatu mfululizo.

## 4.5 Taratibu za Kutoa Korosho Ghala la mnada.

4.5.1 Mnunuzi anaruhusiwa kuhakiki ubora wa korosho alizonunua mnadani na kulipia kablaya kuzitoa katika ghala la mnada kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika mwongozo huu. Mtaalamu wa ubora wa mwendesha ghala ni mhusika mkuu na mtaalamu wa ubora wa mnunuzi ni shahidi.

4.5.2 Mnunuzi anaruhusiwa kuwa na mtaalamu wa ubora aliyepitia mafunzo ya uhakiki Ubora wa Korosho ghafi msimu wa 2021/2022 yaliyotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania, atakayemuwakilisha katika ghala la mnada wakati wa uhakiki wa ubora wa Korosho ghafi kabla ya kuzitoa ghala la mnada.

4.5.3 Mnunuzi atapewa korosho kwenye ghala la mnada kwa kuzingatia daraja la korosho alizonunua mnadani. Fomu maalumu inayoonyesha ubora wa korosho alizochukua iandaliwe na Mwendesha ghala husika, Mnunuzi apewe nakala halisi na Mwendesha ghala abaki na nakala.

4.5.4 Mnunuzi yoyote atakayeshiriki na kuthibitika kuchangia kushuka kwa ubora baada yakukabidhiwa Korosho katika ghala la mnada au kuongeza kitu chochote ambacho sio Korosho atawajibika kwa mujibu wa kifungu cha 23(b) cha Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009.

### 4.6 Sifa za Ghala la Kuhifadhia Korosho

4.6.1 Ghala linapaswa kuwa na milango angalau pande mbili za kuta na madirisha madogo "vents"za kutosha juu na chini kurahisisha mzunguko wa hewa ghalani. Pale itakapobainika kuna uhaba wa maghala bora ya kuhifadhi korosho, bodi ya korosho inaweza kutoa idhini kwa ghala zenye mlango upande moja na madirisha madogo "vents" za juu pekee za kutosha kutumika kuhifadhi korosho ghafi kwa kuzingatia taratibu sahihi za upangaji wa korosho.

4.6.2 Ghala liwe na chaga "pallets" za kuwekea korosho ghafi.

4.6.3 Ghala liwe na sakafu ya saruji iliyo safi.

4.6.4 Ghala halipaswi kuvuja au kuingiza maji wakati wa mvua.

4.6.5 Ghala liwe na vifaa vyote vya ubora kama vilivyotajwa katika kipengele 4.3 vinavyofanyakazi vizuri na vilivyoidhinishwa na mamlaka husika na kuthibitishwa na Bodi ya Korosho.

4.6.6 Ghala linapaswa kuwa na sifa zote kama zinavyoelekezwa na Bodi ya Stakabadhi za Ghala.

### 4.7 Udhibiti Ubora wa Korosho Ghafi ngazi ya Msafirishaji

4.7.1 Msafirishaji anawajibika kuwa na nyaraka zote zinazotambulika kisheria za gari husika linalotumika kubeba korosho ghafi katika msimu 2021/2022.

4.7.2 Msafirishaji akishakabidhiwa korosho ghafi katika ghala la mnada atawajibika kulinda na kutunza ubora na uzito wa korosho hizo hadi kwenye ghala la mnunuzi, bandarini au kiwandani.

4.7.3 Msafirishaji yoyote atakayeshiriki na kuthibitika kuchangia kushuka kwa ubora baada ya kukabidhiwa korosho kutoka ghala la chama cha msingi au ghala la mnada au kuongeza kitu chochote ambacho sio korosho atawajibika kwa mujibu wa Sheria za nchi.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU KATIKA KUSIMAMIA UBORA WAKOROSHO GHAFI

### 5.1 Mkulima

5.1.1 Kuzingatia taratibu zote za uvunaji, ukaushaji, uchambuaji/ udarajishaji na uhifadhi wa korosho ghafi katika madaraja kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya pili ya Mwongozo huu.

5.1.2 Kupeleka Korosho kwenye ghala la AMCOS, kuhakikisha korosho zake zimekaguliwa kwa kumwaga korosho zote mbele ya mjumbe anayesimamia ubora. Baada ya ukaguzi korosho ziwekwe katika gunia la mkonge/kitani lenye ubora uliopitishwa na TBS na alama za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho na.1.

5.1.3 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.2 Vyama Vya Ushirika Vya Msingi (AMCOS)

5.2.1 Kuajiri karani wa ubora au kuwa na mjumbe wa AMCOS atakayesimamia ubora wa Korosho katika kila ghala la Chama cha Ushirika cha Msingi.

5.2.3 Baada ya ukaguzi wa korosho mkulima apatiwe gunia la mkonge au kitani lenye ubora ulioidhinishwa na TBS na alama za utambulisho kama zilizoainishwa kwenye kiambatisho Na.1 kwa ajili ya kuhifadhia Korosho zake kisha kupokelewa ghala la Chama cha Msingi.

5.2.4 Kuhakikisha ghala linalotumika kupokelea korosho kutoka kwa wakulima lipo katika hali nzuri na halivuji.

5.2.5 Kuhakikisha magunia yote yameandikwa au yamechapishwa alama za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho Na.1 kabla ya kusafirishwa kwenda ghala la mnada.

5.2.6 Mjumbe wa Bodi au Mtendaji wa Chama cha Msingi husika ahakikishe Korosho ghafi anazifanyia ukaguzi wa awali wa ubora kabla ya kusafirisha kwenda ghala la mnada.

5.2.7 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.3 Mwendesha Ghala

5.3.1 Mwendesha ghala anapaswa kuwa na vifaa vya ubora kama vilivyoainishwa katika kipengele 4.3 na viwe vimehakikiwa na mamlaka husika (TBS na WMA). Vifaa vyote viwepo ghala la mnada kabla ya zoezi la kupokea Korosho kuanza.

5.3.2 Mwendesha ghala lazima awe na wataalamu wa ubora wa Korosho angalau wawili waliosajiliwa na kupata kibali toka Bodi ya Korosho Iwapo kutatokea uhitaji wa mabadiliko yoyote ya mtaalam wa ubora kwenye ghala la mnada Bodi ya Korosho Tanzania ipatiwe taarifa kwa maandishi.

5.3.3 Mwendesha ghala ahakikishe ghala lake lina sifa zilizotajwa katika kipengele 4.6.

5.3.4 Mwendesha ghala atawajibika kukagua magunia ya korosho anayopokea kwenye ghala la mnada na kuhakikisha yana alama

za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenyekiambatisho Na.1.

5.3.5 Mwendesha ghala anapaswa kupokea korosho zenye ubora unaotambulika na sheria yatasnia ya Korosho kama ilivyoelezwa katika kipengele 4.4.4.

5.3.6 Kutunza Korosho za wakulima na kutoa korosho kwa wanunuzi kwa kuzingatia daraja la ubora alilonunua kwenye mnada na kwa kuzingatia mwongozo huu.

5.3.7 Kuzingatia "First in First Out" (FIFO) wakati wa kutoa korosho katika ghala la mnada.

5.3.8 Kuhakikisha mnunuzi anahakiki ubora kabla ya kuchukua Korosho kwenye ghala la mnada na kusaini kuwa amechukua Korosho zenye ubora kama ilivyobainishwa kwenye stakabadhi husika na kipengele 4.5.3 kwa kuzingatia vigezo vilivyobainishwa katika mwongozo huu.

5.3.9 Kuhakikisha wataalamu wa ubora ghalani maslahi yao yanazingatiwa kwa mujibu wa maelekezo wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

5.3.10 Iwapo kutatokea malalamiko ya ubora kutoka kwa mnunuzi Mwendesha ghala atagharamia shughuli yote ya ubora itakayofanywa na timu ya ubora itakayoundwa kwa zoezi hilo.

5.3.11 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.4 Wanunuzi wa Korosho Ghafi

5.4.1 Kujiridhisha na ubora wa Korosho alizonunua kabla ya kuzitoa ghala la mnada. Endapo, pande zote mbili (Mwendesha Ghala na Mnunuzi) hawatakubaliana utaratibu wa kupima au matokeo ya ubora, anayepinga atatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi Bodi ya KoroshoTanzania.

5.4.2 Mnunuzi akishachukua mzigo ghala la mnada atawajibika kusimamia usafirishaji wa Korosho hizo na kuhakikisha analinda na kutunza uzito na ubora wa Korosho alizotoa katika ghala la mnada.

5.4.3 Mnunuzi atawajibika kuhakikisha Korosho zinasafirishwa zikiwa na magunia yenye alama za utambulisho kama zilizoainishwa kwenye kiambatisho Na.1, ili kurahisisha mfumo wa ufuatiliaji "traceability". Endapo atahitaji magunia ya ziada atalazimika kununua kutoka Chama Kikuu cha Ushirika.

5.4.4 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.5 Wasafirishaji wa Korosho Ghafi

5.5.1 Msafirishaji anatakiwa kuhakikisha anasafirisha korosho katika hali ya usalama bilakuharibu ubora wa korosho hizo.

5.5.2 Msafirishaji anatakiwa kuhakikisha korosho hazinyeshewi na mvua katika muda wote wasafari.

5.5.3 Mwakilishi wa Chama na msafirishaji wanatakiwa kufikisha Korosho kwenye ghala la mnada katika uzito na ubora waliopokea kutoka ghala la Chama cha Msingi husika.

5.5.4 Mwakilishi wa mnunuzi na au msafirishaji anatakiwa kufikisha korosho bandarini au ghala la mnunuzi katika uzito na ubora waliopokea kutoka ghala la mnada.

5.5.5 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.6 Halmashauri

5.6.1 Maafisa kilimo wa kata na kijiji husika wanatakiwa kutoa elimu ya uvunaji, ukaushaji, uchambuaji na uhifadhi wa korosho kwa wakulima wa eneo husika ili kuzingatia ubora katika ngazi ya mkulima.

5.6.2 Maafisa kilimo/ugani wa kata wanatakiwa kufanya ukaguzi kwenye ghala za AMCOS kuhakiki kama ukaguzi wa awali wa korosho za wakulima unafanyika kwa kuzingatia Mwongozo huu.

5.6.3 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.7 Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)

5.7.1 Kukagua na kuthibitisha mizani itakayotumika kupima Korosho.

5.7.2 Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kusuluhisha migogoro inayotokana na vipimo.

## 5.8 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

5.8.1 Kuhakikisha kwamba ghala linalopewa leseni ya kuhifadhi Korosho linakidhi viwango vyote vya kuhifadhi Korosho ghafi kwa kuzingatia mwongozo huu.

5.8.2 Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote kwenye ghala la mnada.

5.8.3 Kumwajibisha mwendesha ghala endapo atabainika kupokea au kutoa korosho zilizo chini ya kiwango.

5.8.4 Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni ya stakabadhi za ghala.

5.8.5 Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.9 Bodi ya Korosho Tanzania

5.9.1 Kufanya ukaguzi wa vifaa vya ubora kabla na wakati wa msimu.

5.9.2 Kufanya ukaguzi wa ghala za minada na shughuli nyingine za utendaji wa mwendesha ghala kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

5.9.3 Kuratibu na kutoa mafunzo ya ubora kuanzia ngazi ya mkulima, Viongozi wa AMCOS na kutoa vibali kwa wataalamu wa uhakiki ubora wa korosho ghafi katika ghala la mnada.

5.9.4 Kutoa vitabu vya hati ya uhakiki ubora wa korosho kwa mwendesha ghala.

5.9.5 Kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika ghala za Vyama vya Msingi kwa kushirikiana na Maafisa ushirika wa Wilaya husika na Ukaguzi ghala za mnada kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala ili kuhakikisha sheria na taratibu za ubora zinafuatwa.

5.9.6 Kutatua migogoro ya ubora pale inapotokea katika mnyororo wa mauzo.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0 UTATUZI WA MIGOGORO

6.1 Changamoto ya ubora itakapotokea katika ghala la mnada taarifa ya maandishi itumwe Bodi ya Korosho ndani ya saa 48 tangu kutokea changamoto.

6.2 Bodi ya Korosho itashughulikia changamoto hiyo kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (e) cha Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 na kutoa maamuzi.Uamuzi wa Bodi ya Korosho utakuwa wa mwisho

***Mwongozo huu unatakiwa kusomwa sambamba na sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 (Tangazo la Serikali Na. 420 la mwaka 2010). Atakayekiuka matakwa ya mwongozo huu atakuwa anatenda kosa hivyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.***

**Mwongozo huu umetolewa: 15 Septemba, 2021**

**Francis Alfred**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

## VIAMBATISHO

***Kiambatisho Na.1***

### RANGI NA ALAMA ZA MAGUNIA YA KOROSHO GHAFI MSIMU WA 2021/22

| S/N | Jina la Chama Kikuu | Rangi ya Majina ya Utambuzi | MKOA | Jina kwa kila gunia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TANECU Limited | Nyekundu | Mtwara | MTW/TANECU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 2. | MAMCU Limited | Bluu | Mtwara | MTW/MAMCU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 3. | RUNALI Limited | Zambarau | Lindi | LND/RUNALI/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 4. | LINDI MWAMBAO Limited | Njano | Lindi | LND/LINDI MWAMBAO/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 5. | TAMCU Limited | Nyeusi | Ruvuma | TNDR/ TAMCU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 6. | CORECU Limited | Kijani | Pwani | PWN/CORECU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 7. | TACACU Limited | Nyeupe | Tanga | TNG/TACACU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |

**NB:** Magunia yote yataandikwa:-Cashewnut Produce of Tanzania